

Shule inatengeneza mipaka – Sisi hatufuati mfumo huo – Schule zieht Grenzen- wir ziehen nicht mit!

Siku mojatulikuwa tumekaa kwenye meza ya chakula iliyoandaliwa vizuri kwa kuwekewa chakula tofauti tofauti, na tulijiuliza: Vitambulisho vina maana gani katika maisha yetu hapa Ujerumani? Sisi ni watu tunaofanya utafiti na kujihusisha na taasisi kama Jugendliche ohne Grenzen, IniRromnja, International Women Space na Verwobene Geschichten.

Tulikuwa na mambo mengi ya kuzungumzia. Wengine pia wageweza kuwa na hoja za kuzungumzia: Vitambulisho vina maana gani katika jamii husika? Je, ilikuwaje hapo zamani? Kuna vizuizi gani kwa baadhi ya watu vinavyosababisha ukosefu wa elimu, kazi, makazi, uhuru wa kutoka sehemu moja kwenda nyingine, na kujumuika katika jamii? Je, ilikuwaje hapo zamani?

Hii ni mada kubwa! Ili kuingalia mada hii kwa ukaribu zaidi, tuliamua kujikita kwenye shule. Hii ni kwa sababu kila mmoja wetu alishawahi kujihusisha na shule katika namna moja au nyingine: Baadhi hawakuweza kusoma shule kwa muda kadhaa; na wengine ilwalazimu kusoma katika shule fulani lengwa; pia wengine walikuwa wanasoma katika madarasa tofauti. Tulibadirishana mawazo na uzoefu wetu juu ya suala la ubaguzi wa rangi mashuleni: Je, tuliwahi kukumbwa na jambo gani shuleni? Ni mada zipi zilikuwa zikishughulikiwa na ni zipi zilikuwa hazishughulikiwi? Je, mada hizi zilikuwa zikiongelewaje? Ni ujuzi gani ulikuwa ukifundisha na ni ujuzi upi ulikuwa haufundishwi? Uhusiano kati ya wanafunzi kwa wanafunzi pamoja na walimu wao ulikuwaje? Je, walimu walizingatia kuwafundisha na kuwachukulia watoto wote sawa? Je, walimu waliichukuliaje hali ya kwamba tulikuwa na vitambulisho tofauti (au hata wengine hatukuwa navyo)? Ilitusaidiaje shuleni kuwa na uwezo wa kujua lugha zaidi ya moja? Je, walimu walilichukuliaje suala la sisi kuwa na dini tofauti – au kuwa wapagani? Ilikuwa inachukuliwaje shuleni, kama mwanafunzi akiwa na ujuzi juu ya sehemu mbali mbali za dunia? Ni lini na vipi walimu walianza ghafla kufuatilia mwonekano wetu, nywele zetu, rangi ya ngozi, umbo na rangi ya macho, hata pua zetu? Ni lini mitandio (vilemba) vilianza kuwa hoja ya kuzungumziwa katika taratibu za shule na kwenye vipindi vya mafunzo? Tangu lini walimu walianza kuongea nasi kwa kutumia kauli za kuonesha utofauti kama »ninyi« (kundi la watu wenye rangi au utafiti tofauti) »Kwenu« (watu kutoka nchi au bala tofauti)? Lini tulikaa kimya na lini tuliendelea kuzungumza? Je, tulijisimamia na kujitetea vipi juu ya ukosefu wa haki?

Ni maswali mengi sana! Kwa ajili ya maonyesho tulikuwa makini kwenye hatua za kwanza: Upatikanaji wa shule kwa ajili ya watoto, vijana na walimu wanaochukuliwa kama wageni (wahamiaji). Tuliuliza: Ina maana gania kama hawa watu wanabaguliwa na kuonekana kama wahamiaji? Je, hali hii inawapa kizuizi gani cha kwenda shule kama watu wengine? Je, wanafunzi na wazazi wao, walimu na jamii yote kwa ujumla inalimudu vipi suala hili la kutotendewa haki?

Tunafurahi ya kwamba chuo kikuu cha *Alice-Salomon-Hochschule* pamoja na Chuo kikuu cha *Hochschule für Technik und Wirtschaft* kwa kushirikiana na *RomaniPhen Archiv*, *Judischen Museum* na *FHXB- Museum* iliyopo kwenye taasisi ya *Institut für angewandte Forschung*. Taasisi tajwa zilitoa mchango wa pesa kwa ajili ya mradi wa utafiti uitwao *Passkontrolle!*

Leben ohne Papiere in Geschichte und Gegenwart. Kwa kushirikiana na *Jugendliche ohne Grenzen*, *IniRromnja*, *International Women Space* na *Verwobene Geschichte* tuliweza kuyafanyia utafuti maswali yetu na kuyaweka wazi majibu ya utafiti wetu kwenye kadamnasi katika maonyesho.

Usiharibu utaratibu – ~~Nicht~~ die Ordnung vereiteln

Mfumo wa shule kwenye ›makoloni ya kijerumani‹ uliwatenga wanafunzi kwa kufuatisha ›rangi za ngozi‹ na ›jinsia‹. Mambo yaliyofundishwa ni yale yaliyoufaidisha utawala wa kikoloni na walowezi wa kizungu tu. Hali hii iliwafanya watu wapinge.

Picha 1: Shule za kimisionari kwa watoto weusi ›German Southwest Africa‹, nchi inayojulikana kama Namibia leo, o.j. © kumbukumbu ya picha imetolewa Deutschen Kolonialgesellschaft, Universitätsbibliothek Frankfurt am Main

Picha 2: Mwanafunzi aliyesoma katika shule ya kimisionari na mpigania uhuru

Hendrik Witbooi hupewa heshima katika *bunge la Gardens Windhoek*, nchini Namibia. Picha hii ilipigwa mnamo mwaka 2016. © Pemba.mpimaji

Picha 3: Mwanafunzi aliyesoma katika shule ya kimisionari na mpigania uhuru Samuel Maharero hupewa heshima jijini Okahandja, nchini Namibia. Picha ilipigwa mnamo mwaka 2006. © bries

Katika sehemu zilizojulikana kama ›makoloni ya kijerumani‹ barani Afrika (1884-1918), maisha ya idadi ya watu weusi yalisifika kwa ubaguzi wa rangi na ukandamizwaji uliofanywa na mfumo wa kikoloni. Kwa idadi ya waafrika, mfumo wao wa kijamii, lugha zao, tamaduni zao na ujuzi wao vilibadirishwa na badala yake iliwekwa mifumo inayousaidia utawala wa kikoloni, walowezi na makampini ya biashara. Mambo haya yote yalifanyika kwa ukatili wa wazi wazi, pia yalifanyika kwa udanganyifu na mbinu nyingine. Hii inathibitishwa na hoja za kibaguzi zisemazo waafrika wanapaswa kustaarabika, kumwamini Mungu na kuelimika.

Shule za kimisionali zilikuwa na maana kubwa katika utekelezaji wa wa miradi ya kikoloni. Kuna shule za watoto *wazungu* na shule za watoto weusi, mafunzo ya wavulana* na wasichana*. Pamoja na kufundishwa hesabu za msingi, kusoma na kuandika, wavulana* walifundishwa kazi za mikono na kilimo, wasichana* walifundishwa kazi za nyumbani ili waweze kufanya kazi kwenye mashamba ya walowezi* wa *kizungu*. → **Das europäische nicht als Vorbild nehmen**

Familia za watu weusi wakiwemo watoto na watu wazima hazipendelei kusoma kwenye shule za kimisionari. Mafunzo yake yanawazuia watoto kufanya shughuli zao za kawaida. Katika shule za wazungu, hawajifunzi mambo wanayohitaji kujifunza wala hawajifunzi mambo wanayopenda kujifunza na hawajifunzi sinsi wanavyopaswa kujifunza katika jamii zao. Kwa kusoma katika shule za kimisionari watoto wanakuwa hawajumuiki katika umoja wa jamii.

Watoto na wazazi wao wanapinga ukatili ambao unatumika kulazimisha watu kwenda shule katika ›Makoloni‹

Baadhi ya watoto na vijana weusi, wengi wao wakiwa wavulana* wanaotoka katika familia zenye ushawishi mkubwa katika jamii, wana nafasi ya upendeleo ya kusoma ya sekondari. Shuleni huko wanaandaliwa kufanya kazi ya upatanishi kati ya watu wa jamii ya kiasia na watawala wa ukoloni wa kijerumani. Wengine wanapelekwa nchini Ujerumani kusoma shule au kupata mafunzo ya elimu ya juu.

Baadhi ya wahitimu* wa shule za sekondari za kimisionari wanatumia elimu waliyoipata kuupinga mfumo wa kikoloni na ubaguzi wa rangi. Wanafunzi wawili waliowahi kusoma katika shule ya kimisionari, waliongoza mgomo kwa kutumia silaha katika ›German Southwest‹, ambayo ni Namibia ya leo: Samuel Maharero, kiongozi wa siasa wa kabila la OvaHerero, na Hendrik Witbooi, kiongozi wa siasa na dini wa kabila la Nama.

Pia wavulana* na wasichana* wa Bonamanga walisoma katika shule za kifalme za kijerumani nchini Kameruni, na baadaye wakiwa watu wazima walitumia ujuzi wao kupiga vita dhidi ya unyonyaji wa kikoloni na ukandamizaji. → **Rudolph Douala Manga Bell**

Nani ni hatari kwa nani?! – Wer ist für wen eine Gefahr?!

Kipindi cha ujamaa wa kitaifa (National socialism), wanafunzi* wa kiyahudi, weusi, wasinti* na waruma* walikuwa wanakosa nafasi ya kwenda shule.

Picha 1: Picha ya mwaka 1905 inaonyesha watoto wa Berlin wakiwa njiani kuelekea shule. Ujamaa wa kitaifa (National socialism) utapunguza mchangamano wa wanafunzi* hawa.
© Gemeinfrei

Picha 2: Shule usharia wa kiyahudi yenye anwani Rykestraße 53, Berlin-Prenzlauer Berg, wakati wa sherehe za michezo mnamo 1938 © Landesarchiv Berlin

Picha 3: Kambi ya kazi za kulazimishwa (forced labor camp) Berlin-Marzahn ilikuwa na shule katika kambi ya jeshi, 1936. © Landesarchiv Berlin

Ulazima wa kwenda shule ni kwa ajili ya watoto na vijana wenye utaifa wa kijerumani chini ya ujamaa wa kitaifa. Uraia unaweza kunyang'anywa au kutopatikana kabisa kwa mtu aliyeuomba hii ni kutokana na sababu za ubaguzi wa rangi au kisiasa, ulazima wa kwenda shule hauhusiki kwa watoto wa familia zisizokuwa na uraia.

Wasinti* na warumi* wa Berlin wanafukuzwa mnamo mwaka 1936 kwenda katika Kambi ya kazi za kulazimishwa wilaya ya Marzahn. Wanafunzi wa shule wanafundishwa katika kambi ya jeshi mpaka mwalimu anapoondolewa, hivyo hawawezi kwenda tena shule. Watoto na vijana kuanzia miaka 12 wanalazimika kufanya kazi za kulazimishwa. Wafanyakazi wa ›Racial Hygiene Research Center‹ wanawafanyia ›uchunguzi‹ wa kisayansi uitwao pseudoscientific na wanakusanya ripoti zijulikanazo kama ›ripoti za rangi za ngozi‹ (race reports). Ripoti hizo zina mchango mkubwa katika kuamua ni watu gani waliomo kambini watafukuzwa. → **Otto Rosenberg**

Mwanzoni, watoto wa kiyahudi wanaruhusiwa kusoma katika shule ya msingi. Kuna Sheria inayoweka mipaka ya kiwango cha nafasi za masomo kwa wanafunzi wa kiyahudi wa vidato vya juu (high school) na vyuo vikuu. Kwa sababu ya mipaka hiyo wanafunzi hao wanalazimika kusoma katika shule binafsi za kiyahudi. Baada ya Kristallnacht mwaka 1938, watoto na vijana wa kiyahudi nawanakatazwa kuhudhulia katika shule za serikali. → Anna Boros

Mwaka 1941 National socialists* walitoa tamko kwamba watoto na vijana wa kisinti*, kiruma*, na wanafunzi weusi wanapaswa kufukuzwa shule pindi watakaposababisha »hatari au madhala kwa wanafunzi wenzao wenye damu ya kijerumani«. Watoto wa kisinti* na kirumi* waishio Berlin hawaathiliwi na tamko hilo tena: Katika wakati wa tamko hili ni kitambo walikuwa wamefungwa katika kambi ya kazi za kulazimishwa (forced labor camp) wilayani Marzahn. Mnamo mwaka 1942 shule zote za kiyahudi zilifungwa na watu wa National socialist*.

»Jana ushirikiano – leo kufukuzwa nchini« - »Gestern Intergration – heute Abschiebung«

Kipindi cha miaka ya 1970 na 1980 kuliwekwa na sheria katika Ujerumani ya magharibi na Berlin ya magharibi, sheria hii ilisababisha utangano wa shule na kutopata haki sawa kwa watoto na vijana wasiokuwa na utaifa wa kijerumani. Kulikuwa na kukosoa na kupinga.

Picha 1 na 2: Maandamano ya haki sawa mashuleni na upatikanaji wa nafasi za mafunzo ya vyuoni. Picha hizi zilipigwa Kottbusser Damm mjini Berlin ya magharibi, 1975. © Jürgen Henschel

Picha 3 na 4: Maandamano dhidi ya sheria iliyowekwa iliyosababisha upatanisho wa familia kuwa mgumu na kurahisisha ufukuzwaji wa vijana. Picha hizi zilipigwa Hermannplatz mjini Berlin ya magharibi, 1981. © Jürgen Henschel

Kutenganishwa kwa mashule na kutotendewa haki kulileta hathari kubwa sana hasa watoto wa wahamiaji* (wageni). Wanaruhusiwa kuhudhulia darasa la kwaida kama idadi yao ya darasani iko chi ya asilimia 20 %, kunzia mwaka 1982 idadi yao ya darasani iwe chi ya asilimia 30 %. La sivyo watafundishwa katika madarasa yaitwayo »Ausländer-Regelklassen« (madarasa ya wahamiaji). Wanafunzi* wasiojua lugha ya kijerumani wanawekwa kwenye madarasa ya awali na kwa takribani baada ya miaka miwili wanavushwa kwenda darasa la kawaida. Kiukweli wanabakizwa katika darasa la awali kwa muda mrefu. → Figen Izgin

Kwa mujibu wa ofisi ya wilaya, Wanafunzi* wenye umri zaidi ya mika 14, wanapoingia nchini ujerumani na kushindwa kumaliza na kufaulu masomo ya darasa la kumi ndani ya miaka miwili, watalazimika kuhudhulia mafunzo yaitwayo »Eingliederungslehrgänge« (integration courses) na hawatahesabika kama wahitimu wa shule. Tangu mwaka 1984, watoto na vijana ambao wako kwenye mchakato wa kuomba vibali vya kuishi ujerumani

kama wakimbizi wana haki ya kwenda shule. Ili mtoto aweze kuhudhlie shule, ni lazima wazazi wake watume maombi. Kwa kuwa wazazi hawana taarifa za kutosha, maelfu ya watoto wamekuwa wakikosa elimu kwa miaka mingi.

Mara kwa mara, watoto wa wafanya kazi wa kigeni pamoja na watoto na vijana wenye vibali vya makazi maalum au wanaoomba vibali vya kuishi nchini kama wakimbizi wanaagizwa kumasoma katika (an Haupt- und Sonderschulen) shule za sekondari na shule maalum au wanaacha shule bila kuhitimu.

Kupitia maandamano, wazazi, wanafunzi* na mashirika (ya kigeni) yasiyo ya kiserikali yanajaribu kulalamika mahakamani na kuandika barua za malalamiko dhidi ya mipaka iliyotengenezwa na ubaguzi wa rangi katika upatikanaji wa elimu ya shule. Wanakosoa nafasi mbovu za elimu na kazi, Wanadai uwepo wa shule zitumiazo lugha zaidi ya moja (multilingual) katika ufundishaji na mtaala unaolenga tamaduni mbali mbali na kurejea katika historia ya wanafunzi. Wakati huo huo, wanapinga ukusefu wa ulinzi wa kihamiaji kwa watoto na vijana na dhidi ya kufukuzwa nchini.

Jinsi Aussiedler* (wajerumani wanaohama kutoka nchi nyingine kurudi Ujerumani) wanavyopewa haki sawa kama wajerumani wengine, imeonyesha kwamba njia nyingine tofauti inawezekana kama kuna utayari wa kisiasa. Kwa mfano, watoto na vijana wa kijerumani wanaohama kutoka nchi nyingine kurudi Ujerumani, hawapati tu makazi yenye ulinzi kwa haraka sana, bali wanakubalika kusoma katika madarasa ya kawaida. Kwa wasiozungumza lugha ya Kijerumani wanapata mafunzo ya ziada.

Haki sawa kwa wote?! – Gleiche Recht für alle?!

Mara kwa mara utengano wa mafunzo mashuleni unakomeshwa – na unarudishwa tena kwa njia ya maandamano. ›wenye vibali vya makazi maalum‹ na watoto na vijana wasiohalalishwa kuishi Ujerumania wanaendelea kupigania haki zao.

Picha 1: *Wote wanabaki!* Maandamano ya mwaka 2011 mjini Wiesbaden katika hafla za kongamano la mawaziri wa mambo ya ndani. © alle bleiben! → *alle bleiben!*

Picha 2: *Jugendliche ohne Grenzen* waliandamana mwakad 2014 mjini Bonn katika hafla za kongamano la mawaziri wa mambo ya ndani. © Jugendliche ohne Grenzen → *Jugendliche ohne Grenzen*

Picha 3: Kipeperushi cha maandamano cha *IniRromnja* kinachohusu uamuzi wa kisiasa juu ya *Berliner Aktionsplan* (mpangi wa vitendo mjini Berlin) unaothibitisha ushiriki wa Roma ya kigeni katika ›Willkommensklassen‹ (madarasa ya kukaribisha). © Nihad Nino Pušija → *Romano-Bündnis*

Watoto na vijana wenye vibali vya makazi maalum au wanaoomba vibali vya kuishi nchini kama wakimbizi katika mkoa wa Berlin, wanalazimika kwenda shule kutokana na sheria iliyotungwa tangu mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990's). Lakini mashirika yasiyo ya

kiserikali kama Initiativen *Jugendliche ohne Grenzen* na *alle bleiben!* wanaonesha kupitia harakati tofauti yakiwemo maandamano, kwamba kuna vizuizi vingi katika upatikanaji wa elimu, mafunzo ya vyuo na ukosekanaji mkuba wa ulinzi kutokana na hadhi ya makazi. Watoto na vijana wasiohalalishwa kuishi Ujerumania, ambao hawana vibali vya uraia, wanaendelea kuwa na haki ya kuhudhuria shule tu. Lakini hata hivyo ni ngumu kutekeleza katika vitendo. → **Jugendliche ohne Grenzen → alle bleiben!**

Baada ya miaka mingi ya kuandamana kwa wazazi, watoto na mashirika (ya kigeni) yasiyo ya kiserikali walifanikiwa kuondoa ›idadi ya mahudhulio kwa asilimia‹ na ›Darasa la kawaida – kwa wahamiaji‹ mnamo mwaka 1995, na Aussiedler*innen (wajerumani wanaohama kutoka nchi nyingine kurudi Ujerumani) hawakupata tena upendeleo wa kipekee bali walipata haki sawa na wahamiaji.

Mafunzo yaitwayo ›Eingliederungslehrgänge‹ (integration courses) yatasitishwa mwanzoni mwa muhula wa 1999/ 2000. Utengano wa mafunzo mashuleni haukubaliki tena kwa sababu ya uraia, lakini bado uwepo wake unawezekana kwa sababu ya kutoijua lugha ya Kijerumani. Hatimaye mwaka 2007, watoto wasiojua lugha ya Kijerumani watakuwa wanasajiliwa katika madarasa ya kawaida na watapata mafunzo ya ziada ya lugha ya Kijerumani katika vikundi.

Tangu muhula wa 1997/98, mtoto asiyezungumza kijerumani kama lugha mama ›nichtdeutsche Herkunftssprache‹ (›ndH‹) ananakiliwa wakati wa kujiunga na shule. Hakuna sheria ilinayoeleweka juu ya anayehusika na utaratibu huu, na jinsi ya kuainisha na utaratibu huu hausemi kitu juu ya hitaji lililopo la kutoa msaada katika mafunzo ya lugha ya Kijerumani. Wazazi wengi wanaziepuka shule zinazofuatilia kwa hali ya juu watoto wasiozungumza Kijerumani kama lugha mama ›ndH-Anteil‹. Baadhi ya wazazi, wanajaribu kuulazimisha uongozi wa shule kupunguza idadi ya watoto wasiozungumza Kijerumani kama lugha mama katika madarasani wanayosoma watoto wao ›ndH‹. Pia kuna uongozi wa shule zingine unaotenga madarasa bila kulazimishwa na wazazi wa watoto husika. Kitendo cha kutenga madarasa hakikubaliki kisheria na ikitokea tukio hilo likatolewa taarifa basi litabadirishwa.

Tangu muhula wa 2011/12, kupitia wa mfumo uitwao ›Makundi ya mafunzo kwa ajili ya wanafunzi wapya wasioijua lugha ya Kijerumani‹ (›Willkommensklassen‹) ilihalalishwa tena kisheria kwamba kuwepo na mafunzo katika madarasa yaliyotengwa. Hii inawahusu warumi* wasio na uraia wa Kijerumaniohne na inasababisha kupinga na kuandamana kwa makundi kama (*Romano-Bündnis*). Miaka inayofuata wanafunzi wasioijua lugha ya Kijerumani ›Willkommensklasse‹ wamekuwa wakienda mashuleni kwa wingi, wengi wao wakiwa ni wakimbizi watoto na vijana na wale wanaotokea katika nchi za Ulaya ya kusini. Masomo hayazingatii dhana wala vifaa, hivyo walimu huamua na kupanga masomo yaweje na ni lini mtoto anaweza kuvuka kutoka darasa moja kwenda darasa la kawaida. Mara nyingi masomo hufanyika katika vyumba au majengo tofauti. → **Sabina Salimovska → Tuğba Tanyılmaz → Saraya Gomis**

Na ilikwaje katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani (JKK)? – Und wie war es in der DDR?

Serikali ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani (JKK) ilitengeneza ushirika wa elimu na vyama vya kisiasa vya kigeni na serikali mbali mbali ili wafundisha wanafunzi* kuishi maisha ya ujamaa katika shule za mabweni kwenye Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani (JKK).

Picha 1: Kusimamisha bendera kwenye *Käthe-Kollwitz-Heim* mjini Moritzburg. © SLUB/Deutsche Fotothek, Erich Pohl

Picha 2: Andreas Shiyoo (aliyesimama kati kati, wa tatu kutoka kushoto.) Alikuwa mmoja kati ya watoto 400 kutoka nchini Namibia, waliokulia katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani (JKK). © Andreas Shiyoo

Kama taifa lenye mfumo wa anti-fascist, serikali ya JKK inapinga ujamaa wa kitaifa (National socialism) na ukoloni. Mfumo wa elimu umeundwa kama wa antifascist-democratic na baadaye kama ujamaa. ushirika wa elimu na vyama vya kisiasa vya kigeni na serikali mbali mbali zilizokuwa zinaunga mkona harakati za kuupinga ukoloni na kuchagua kutokuwa na ubepari katika maendeleo ili kujenga nchi yao upya. Mitaala kwa ajili ya wanafunzi* inatengenezwa na shule za mabweni zinajengwa.

Baada ya Vietnam ya kaskazini kujitenga na utawala wa ukoloni wa Ufaransa, inaweka makubaliano na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani JKK mnamo mwaka 1955: watoto 350 wa waliokuwa wanajeshi* waliokuwa wanapigana vita na utawala wa ukoloni wa Ufaransa wanaishi na kusoma kwenye *Käthe-Kollwitz-Heim* mjini Moritzburg. Mpaka leo wanajiita »Moritzburger« (watu wa Moritzburg).

Jamuhuri ya Msumbiji pia inaingia katika makubaliano ya mkataba na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani. Kutokana na nafasi tofauti tofauti za ushirika wa elimu kimataifa, Msumbiji inachagua kushirikiana na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kijerumani. Mwaka 1982, watoto 899 wa Msumbiji wanaingia katika JKK na wanasoma katika *Schule der Freundschaft* mjini Staßfurt. Shule hii ya bweni ilijengwa maalum kwa ajili yao, ilikuwa ni nyumbani kwao kipindi cha wiki nzima (kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi) hadi mwaka 1988. Kipindi cha wikiendi na kipindi cha likizo, wanafunzi* walikwenda kukaa na familia zilizowaalika mjini humo na maeneo ya karibu na mji huo. Lakini lengo la kuwaandaa watoto kwa ajili ya kujenga Msumbiji kama nchi ya Ujamaa halikufaulu: Baada ya mabadiriko katika siasa ya uongozi wa nchi, Msumbiji haiyatambui mafunzo waliyofuzu watoto katika JKK.

Pia vijana kutoka Namibia wanaishi kwa muda katika *Schule der Freundschaft* na wanasoma katika chuo cha ufundi *Willy Wallstab* mjini Löderburg katika darasa lao peke yao. Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi* wa Msumbiji, mtaala na dhana zinazotumika katika kuwafundisha vinachukuliwa kutoka katika lugha, utamaduni na utamaduni wa asili yao. → »DDR-Kinder« aus Namibia

Kutenganishwa kwa shule katika JKK kulitegemeana na makubaliano kati ya nchi zilizoingia mkataba na JKK. Wanafunzi* wengine, waliokuwa wanakaa kwa muda mrefu katika JKK, walisoma katika madarasa ya kawaida katika mfumo wa shule za kawaida (zisizotenganisha madarasa). Japo mfumo uliowekwa (wa elimu ya ushirikiano) ulikuwa unazingatia usawa na mshikamano haimaanishi kwamba mtaala, mawasiliano na maisha ya kila siku hayakuwa na ubaguzi wa rangi. Hata kama sera ya utambulisho wa taifa haikuhusika katika ukoloni na ujamaa wa kitaifa (Nazism) na kutoyataja mambo haya darasani au sehemu yoyote ile, hali hii ina madhara – siyo kwa wanafunzi* tu bali na kwa walimu* wa rangi.

Anna Boros

"Nilikatazwa kwa nguvu kutofanya mafunzo niliyopendelea kusoma chuoni."

Picha 1: Anna akiwa na mama yake (Julie) pamoja na mume wa mama yake (Georg) wakiwa sebuleni mwao mjini Berlin, 1936. © Yad Vashem, The Righteous Among Nations Department

Picha 2: Kwa takribani miaka kumi, pindi mfumo wa Nazism (ujamaa wa kitaifa) ulipofikia kikomo, Anna Gutmann anayejulikana kama Anna Boros kabla ya kuolewa, alipigania haki yake ya kupata fidia ya viziwi vilivyokuwepo katika »upatikanaji wa nafasi ya kazi aliyoitaka yeye«. 1954. © LABO

Picha 3: baada ya kifo chake Dr. Mohamed Helmy alipewa heshima ya » Uadilifu miongoni mwa mataifa« (Gerechter unter den Völkern) kwa sababu aliokoa maisha ya Anna. Pichani anaonekana mpwa wa Helmy aitwaye Dr. Nasser Kotby (Misri) na binti yake Anna aitwaye Carla Greenspan (USA) wakiwa katika sherehe mjini *Yad Vashem*, Magharibi mwa Yerusalemu, 2013. © Yad Vashem, The Righteous Among Nations Department

Anna Boros anazaliwa mwaka 1925 mjini Arad nchini Romania. Baada ya wazazi wake kutengana yeye pamoja na mama yake wanahamia kwa bibi yake mjini Berlin. Maisha ya familia yake yanabadirika mara tu baada ya National Socialists* (Wafuasi wa ujamaa wa kitaifa) kuwa na nguvu kubwa ya kisiasa mnamo mwaka 1933: Anna, mjomba wake aitwaye Martin na bibi yake aitwaye Cecile Rudnik wananyang'anywa kibali cha makazi. Mama yake Annas aitwaye Julie ananusulika kunyang'anywa uraia wake kwa sababu ameolewa na Georg Wehr, *mzungu* wa kijerumani aliyebadilisha dini yake kutoka Ukristo kwenda Uyahudi. Kwa sababu za ubaguzi wa rangi, Georg hakutambulika kama myahudi licha ya kubadili dini, alibaki kuwa mtu mwenye rangi ya aina ya »Aryan«. Baada ya kupata haki ya familia itwayo (patriarchal) mke wa Georg wa kiyahudi ajulikanaye kwa jina la Julie anapata uraia wa kije-rumani. Baadaye George na Julie nao walianza kufuatiliwa na kuwiSpäter.

Bibi Cecile Rudnik ana biashara ya familia katika mtaa wa Neue Friedrichstraße 77. Anaponyang'anywa na kupoteza biashara yake familia haibaki kukosa utaifa tu bali inakuwa masiki-

ni bila kitu chochote cha thamani. Kwa sababu ya sheria ya utawala wa National Socialism, Anna hawezi kwenda shule tena na hawezi kuhitimu mafunzo yoyote ya chuo. Ndoto yake ya kuwa muuguzi wa watoto ambayo inawezekana kupitia kituo cha watoto yatima wa kiyahudi inakatishwa kwa sababu taasisi zote za kiyahudi zinafungwa.

Kupitia unyang'anyi wa biashara ya familia yake, Anna hawezi kufanya kazi katika biashara hiyo, hivyo anapoteza nafasi ya mafunzo kwa vitendo. Wayahudi* wanapoanza kufukuzwa ufuatiliaji wa familia ya Anna unaongezeka kwa kasi: Anna, mjomba wake na bibi yake wanajificha chini ya ardhi mwaka 1942. Daktari wao aitwaye Dr. Mohamed Helmy, Mmisri aishiye mjini Berlin, anaisaidia familia kwa kuipatia chakula na vinywaji wakati wa maficho yao chini ya ardhi. Mwanzo kabisa Anna anaishi katika zahanati yake. Anna hawezi kuitimiza ndoto yake ya kusomea uuguzi wa watoto katika chuo. Si haba, wakati wa maficho yake ana-weza kufanya kazi katika zahanati. → **Wer ist für wen eine Gefahr?!**

Dr. Helmy anaitumia nafasi yake kuwasiliana na wahamiaji wengine wa Kimisri, kwa lengo la kumwezesha Anna Boros kutoroka Ujerumani. Kwa kutumia msaada wa rafiki yake aitwaye Dr. Kamal El-Din Galal (Katibi mkuu wa *makao makuu ya Taasisi ya Kiislam Berlin*) anafanya mpango wa kumbadirisha Anna dini kuingia Uislamu. Rafiki yake mwingine ambaye ni mwanamuziki aitwaye Abdel Aziz Helmy Hammad, anakubali kufunga ndoa ya uwongo na Anna, hatimaye Anna anapewa jina la Kiislamu na kuitwa Nadiya, baada ya sheria ya Kiislamu iitwayo (Sharia). Baada ya kuhalalishwa kwa ndoa yake kupitia mamlaka ya kije-rumani angeweza kunufaika kwa kupewa utaifa wa mumewe (Utaifa wa Kimisri) na angeweza kuondoka Ujerumani – hivyo ndivyo mpango ulivyokuwa. Lakini mamlaka haikuitambua ndoa hiyo. Pia jaribio la Dr. Helmys la kumfanya Anna kuwa binti yake wa kufikia (adapt) lilishindikana. Baada ya maficho ya Anna (yaliyokuwa kwenye zahanati iliyokuwa Moabit) kuwa kuwa katika hali hatarishi, Dr. Helmy alimficha Anna kwenye nyumba ndogo iliyoko bustanini mwake (Gartenlaube) wilayani Buch mkoani Berlin.

Anna ananusurika, Hata baada ya mwisho wa National Socialism, hawezi kupata mafunzo ya chuo nchini Ujerumani kwa sababu ya matokeo yaliyosababishwa na mfumo huo wa Nazism, hivyo anaamua kuhamia nchini Marekani (USA).

Otto Rosenberg

"Na mimi pia nilipinga."

Picha 1: Kambi ya kazi za kulazimishwa (forced labor camp) Berlin-Marzahn – mahali pa kumbumbu na taarifa, Landesverband Deutscher Sinti und Roma Berlin-Brandenburg e.V., 2019 © Jolan Attia Cantzen

Picha 2 Kambi ya kazi za kulazimishwa (forced labor camp) Berlin-Marzahn – mahali pa kum-bumbu na taarifa,, Landesverband Deutscher Sinti und Roma Berlin-Brandenburg e.V., 2019 © Jolan Attia Cantzen.

Otto Rosenberg anazaliwa mwaka 1927 katika Prussia ya mashariki na anakulia mkoani Berlin. Mwaka 1936, kipindi cha kiangazi, jeshi la Gestapo lilimfukuza Otto (akiwa na miaka tisa) pamoja na familia yake kwa ujumla kuelekea katika kambi ya kazi za kulazimishwa

wilayani Marzahn mkoani Berlin. Huko analazimika kuishi katika hali ya kinyama, haruhusiwi tena kuhudhulia masomo katika shule ya kawaida na katika hali ya ubaguzi wa rangi ›anapimwa afya yake‹ na ›kufanyiwa uchunguzi‹. → **Wer is für wen eine Gefahr?!**

Akiwa na 13 Otto analazimishwa kufanya kazi katika kiwanda cha silaha za moto za kiji-shi. Kiwandani huko anashutumiwa na anahisiwa hujumu hivyo anafungwa katika gereza la wilayani Moabit mnano 1942, ambako analazimika kukaa kwa muda wa miezi minne katika selo ya peke yake (cellular imprisonment). Kutoka huko, anafukuzwa kwenda Auschwitz mwanzoni mwa mwaka 1943. Kati ya ndugu kumi ni Otto pekee anayenusurika na kifo.

Mara tu baada ya vita Otto Rosenberg anaanza kufanya kazi za kisiasa. Anapigania usawa wa Wasinti* na Warumi* katika jamii na anakuwa sauti muhimu ya harakati za haki za raia. Mwaka 1978 anakuwa mmoja wa waanzilishi* wa *umoja wa wasinti Berlin (Cinti Union Berlin)*, ambayo leo inaitwa *Landesverband Deutscher Sinti und Roma Berlin-Brandenburg*, na anakuwa mwenyekiti wa chama hicho kwa muda wa miaka mingi. Pia ni mwanachama wa bodi ya *Zentralrates Deutscher Sinti und Roma tätig*. Anafariki mwaka 2001 mkoani Berlin.

» Kambi ya shule ilijengwa karibu na kambi ya jeshi la polisi kwa sababu tulikuwa haturu-husiwi tena kwanda shule. Huo ndio ulikuwa mwisho wetu. Tulikatazwa kusoma katika shule kubwa iliyokuwa Berlin-Marzahn, karibu na kanisa la kijiji. Tulikuwa na mwalimu mmoja tu. Tulikuwa wanafunzi wa madaraja (madarasa) tofauti lakini kwa pamoja tulikuwa na vyumba vya viwili tu vya madarasa. Kimoja kilikuwa cha wanafunzi wadogo sana. Tilipewa baadhi ya vitabu bure, lakini tulilazimika kulipa kitu. Tulikuwa na daftari la hesabu, daftari la ziada la kufanyia mazoezi (roughbook), daftari la mwandiko, Kitabu cha mazoezi ya kusoma na kita-bu cha hesabu. Hivyo ndivyo vitu tulivyokuwa navyo, hatukuwa na kitu kingine chochote. Hatukujifunza sana.«

Quelle: Otto Rosenberg (2012): Das Brennglas, S. 21

»Mwalimu aliyekuwa mwenye heka heka (hyped up). Ndiyo? Aliingia darasani na kuchukua kijiti chake cha kufundishia na kutuonyesha mahali jeshi la kijerumani liliko kwa sasa. Lakini hatukutaka kujua jeshi letu liko wapi. Na akaenda kuzungumza na mke wa mkulima amwambia: ›Otto hakikisha wanayanakili mambo yote niliyoandika ubaoni.‹ Hivyo ndivyo ilivyoku-wa. (...) Na kwa mtindo huo mtu hawezi kujifunza kitu.«

Quelle: Interview mit Otto Rosenberg, FU Berlin

»Tangu nikiwa mtoto nilikuwa nabaguliwa, lakini mtoto anaichukulia hali hii tofauti. Na nil-ijitetea. Dhidi ya watoto walionibagua. Mara kwa mara nilikuwa nukuvaa viatu vya mbao (wooden slippers), ninafikiri ni kwa sababu kulikwa hakuna hela ya kununua viatu vya ka-waida. Na nimepata heshima kupitia hivyo viatu vya mbao. Vilifaa sana kwa ajili hiyo. Wato-to walibeba mabegi yao ya shule kifuani. Hivyo walicheza mchezo wa kuendesha ndege, wa-liniparamia na kunifokea pia, walinitukana kwamba mimi ni ~~gypsy~~ mchafu, na mengine men-gi. Ndiyo maana nilishawahi kumpiga mtoto wa askari kwa kutumia viatu vyangu vya mbao.«

Quelle: Otto Rosenberg (2012): Das Brennglas, S. 15–16

Rudolph Douala Manga Bell

"...kwamba hii ardhi haitakanyagwa tena na Wajerumani."

Picha 1: Familia ya Bonamanga, katikati wamekaa wanandoa ambao ni Emily und Rudolph Douala Manga Bell. © Archiv der Basler Mission

Picha 2: Vizazi vitatu vya familia ya Bonamanga wamemtembelea mchungaji ambaye ni rafiki yao, wakati walipokuja Berlin kutetea haki zao, 1902. © Gemeinfrei

Picha 3: Baada ya jumuiya ya watu waishio ugenini (diasporic community) pamoja na watu wanaowaunga mkono* kupigania haki zao kwa muda mrefu, jina la mtaa wa Nachtigalplatz ulibadirishwa jina na kuitwa Manga-Bell-Platz wilayani Wedding mkoani Berlin. © Tahir Della

